



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



Kumb.Na MTC/ C.40/9/28.

22/03/2022

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI
ZA MAKAZI NA POSTIKODI (NAFASI 150)**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya muda nafasi mia hamsini (150) za kukusanya taarifa kwenye zoezi la anwani za makazi katika Kata , Mitaa na Vitongoji vyote vya Halmashauri ya Mji Makambako.

A. SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe Raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18-35
- Awe na Elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
- Awe anamiliki simu janja (android) yenye uwezo wa kukaa na chaji siku nzima.
- Awe na barua pepe (email address) na nywila (password) inayofanya kazi
- Awe na uwezo wa kusoma ramani za mitaa/vijiji
- Awe ni mkazi wa Kata husika.

B. KAZI NA MAJUKUMU

- Kugawa/Kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma.
- Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumuia mfumo wa anwani za makazi (NAPA)
- Kutuma data kwenye mfumo wa anwani za makazi

C. MAOMBI YAAMBATANISHWE NA NYARAKA ZIFUATAZO.:-

- Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- Picha mbili (2) ,(passport size) za hivi karibuni
- Barua ya maombi ipitishwe kwa Mtendaji wa Mtaa/kijiji unapoishi.
- Nakala ya kitambulisho cha uraia (NIDA), kwa ambao bado hawajapokea vitambulisho vya NIDA waandike namba zao za NIDA katika barua za maombi.

Halmashauri ya Mji Makambako, Mtaa wa Sigrid, Barabara kuu ya Njombe, S.L.P 405 Makambako,Njombe, Nukushi Na: 026-2968891, Simu Na: 026-2968892,


Barua Pepe: td@makambakotc.go.tz, Tovuti: www.makambakotc.go.tz

D. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya muombaji, namba ya simu, barua pepe na ziwasilishwe kwenye **OFISI YA MTENDAJI KATA** ambayo muombaji anatokea.

E. TAREHE YA MWISHO KUPOKEA MAOMBI

Mwisho wa kupeleka maombi ni tarehe 25/03/2022. saa 9:30 Alasiri



Kenneth .K. Haule

MKURUGENZI

HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO

MKURUGENZI

HALMASHAURI YA MJI

MAKAMBAKO